ISSN 0856-6976

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

*Mapitio ya Nusu Mwaka*
**2017/18**

**GAVANA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Februari 2018**

**ISSN 0856-6976**

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

*Mapitio ya Nusu Mwaka*

**2017/18**

**GAVANA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

Februari 2018

# Utangulizi

Taarifa hii ya mapitio ya Tamko la Sera ya Fedha inatathmini mwenendo wa utekelezaji wa Sera ya Fedha katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2017/18 na kuainisha mwelekeo wa kisera ambao Benki Kuu inakusudia kuchukua katika kipindi kilichobakia cha mwaka 2017/18.

## Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Kulingana na taarifa ya mwelekeo wa hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mwezi Januari 2018, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2017, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2016. Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia kumechangiwa na kuimarika kwa mahitaji ya ndani na nje yaliyotokana na sera ya fedha na ya kibajeti ya kuongeza ukwasi. Ukuaji wa uchumi wa dunia umechangiwa na nchi zote hasa nchi zinazoibukia kiuchumi, nchi za Umoja wa Ulaya na zile zinazoendelea kukua (*emerging market, Euro area and developing economies*). Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inatarajiwa kuongezeka kufikia wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2018 na 2019. Uchumi wa nchi zilizoendelea na zile zinazoibukia kiuchumi unatarajiwa kuchangia zaidi ukuaji huu kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya ndani yatakayotokana na sera ya fedha na ya kibajeti ya kuongeza ukwasi katika nchi hizo.

Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017/18, mfumuko wa bei uliongezeka katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zile zinazoendelea kukua, hususan kutokana na kupanda kwa bei ya nishati. Katika nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, mfumuko

wa bei ulipungua ukichangiwa zaidi na kupungua kwa bei ya chakula, hali iliyosababishwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula kufuatia hali nzuri ya hewa katika ukanda huo. Kulingana na taarifa ya mwelekeo wa hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mwezi Januari 2018, mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea unatarajiwa kuongezeka na kufikia wastani wa asilimia 1.9 mwaka 2018 ukichangiwa zaidi na bei ya nishati. Wakati huohuo mfumuko wa bei katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zile zinazoendelea kukua unatarajiwa kuongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 4.5 kutokana na kupanda kwa bei za vyakula.

## Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

### Tanzania Bara

Katika kipindi cha robo tatu za mwanzo za mwaka 2017, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 6.8. Shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kasi zaidi ni pamoja na madini kwa asilimia 24.3, mawasiliano (asilimia 13.1), usafirishaji na uhifadhi (asilimia 11.9), maji (asilimia 10.0), viwanda (asilimia 9.8) na ujenzi (asilimia 9.5). Mfumuko wa bei umeendelea kupungua ukichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula, utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani na sarafu nyingine duniani, kuimarika kwa uzalishaji wa umeme na utekelezaji thabiti wa sera ya fedha na ya kibajeti. Mfumuko wa bei wa jumla ulipungua hadi asilimia 4.0 mwezi Desemba 2017 kutoka asilimia 5.4 mwezi Juni 2017, wakati mfumuko wa bei usiojumuisha bei za vyakula na nishati (*core inflation*) ulikuwa chini ya wastani wa asilimia 2.0, ukipungua kutoka asilimia 1.9 mwezi Juni 2017 hadi asilimia 1.3 mwezi Desemba 2017.

Katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2017/18, mapato yaliyokusanywa na kuwekwa kwenye akaunti za Serikali zilizoko Benki Kuu ya Tanzania yalikuwa shilingi bilioni 8,438.7, kiasi ambacho kilikuwa ni asilimia 4.6 zaidi ya mapato yaliyokusanywa na kuwekwa kwenye akaunti hizo katika kipindi kama hicho mwaka 2016/17. Aidha, kiasi hicho ni sawa na asilimia 92.5 ya makadirio ya makusanyo katika kipindi cha miezi sita ya kwanza ya mwaka 2017/18. Kuongezeka kwa makusanyo ya mapato kwa sehemu kubwa kumetokana na jitihada zinazotekelezwa na Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), zenye lengo la kuongeza ukusanyaji wa mapato nchini. Katika kipindi hicho, jumla ya matumizi ya Serikali yaliyofanywa kupitia katika akaunti zake zilizoko Benki Kuu yalifikia shilingi bilioni 8,727.1. Shilingi bilioni 6,774.9 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shughuli za maendeleo ziligharimu shilingi bilioni 1,952.2.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2017/18, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje (*current account deficit*) ilikuwa dola za Marekani milioni 551.2, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 683.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2016/17. Kupungua huko kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje kulichangiwa na kupungua kwa thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya nchi, pamoja na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii na usafirishaji. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,906.2 mwishoni mwa mwezi Desemba 2017, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,000.4 mwishoni mwa mwezi Juni 2017 na dola za Marekani milioni 4,325.6 mwishoni mwa mwezi Desemba 2016. Akiba hii inatosha kulipia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 6.

Deni la sekta ya umma liliongezeka kwa dola za Marekani milioni 1,054.6, kutoka dola za Marekani milioni 19,957.6 mwezi Juni 2017 na kufikia dola za Marekani milioni 21,012.2 mwezi Desemba 2017. Katika kipindi hicho, deni la nje likijumuisha deni la sekta binafsi liliongezeka kwa asilimia 3.4 na kufikia dola za Marekani milioni 19,180.2 mwishoni mwa mwezi Desemba 2017, ikilinganishwa na deni lililokuwepo mwishoni mwa mwezi Juni 2017. Aidha, deni la ndani la Serikali liliongezeka kwa asilimia 8.6 na kufikia shilingi bilioni 12,810.3 mwishoni mwa mwezi Desemba 2017 kutoka shilingi bilioni 11,790.8 mwishoni mwa mwezi Juni 2017. Ongezeko hili lilitokana na uuzaji wa dhamana na hati fungani za Serikali kwa ajili ya kugharamia bajeti ya Serikali.

Sekta ya kibenki imeendelea kuwa imara, salama, na yenye mitaji na ukwasi wa kutosha. Uwiano wa mitaji ya mabenki ikilinganishwa na rasilimali zao (*ratio of core capital to total risk weighted assets and off-balance sheet exposures*) ulikuwa asilimia 18.9 mwezi Desemba 2017, ikiwa juu ya kiwango kinachohitajika kisheria cha asilimia 10.0. Hali ya ukwasi wa mabenki kiujumla imeendelea kubakia kwenye kiwango cha juu cha asilimia 40.3 ikilinganishwa na kiwango kinachohitajika kisheria cha asilimia 20. Wakati huo huo, uwiano wa mikopo chechefu, uliongezeka kufikia asilimia 11.7 mwezi Desemba 2017, kutoka asilimia 10.6 ya mwezi Juni 2017. Hata hivyo Benki Kuu ya Tanzania kama msimamizi wa mabenki, imeagiza benki zote nchini kuweka mikakati imara ya kupunguza mikopo chechefu na imezitaka benki za biashara kuendelea kutumia mfumo wa kuhifadhi taarifa za wakopaji ili kupunguza vihatarishi katika kutoa mikopo mipya kwa sekta binafsi.

Benki Kuu pia imeagiza benki zote nchini kuweka ziada ya kiasi cha mitaji yao kwa ajili ya kupambana na vihatarishi vya kiuendeshaji (capital charge for operational risk) kuanzia mwezi Agosti 2017. Benki zinatakiwa pia kuwa na nyongeza ya asilimia 2.5 ya uwiano wa mitaji yao ikilinganishwa na rasilimali zao ikiwa ni juu ya kiwango kilichowekwa kisheria. Aidha, mwezi Januari 2018, Benki Kuu ilitoa leseni kwa benki moja kuanzisha biashara ya kibenki nchini na kuzifutia leseni za kuendelea kufanya biashara nchini benki tano na kuziweka chini ya ufilisi. Uamuzi huu ulichukuliwa baada ya Benki Kuu kujiridhisha kuwa benki hizo zilikuwa na upungufu mkubwa wa mtaji kinyume na matakwa ya sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na kanuni zake. Upungufu huo wa mtaji ulionekana kuhatarisha usalama wa sekta ya fedha na kwamba kuendelea kutoa huduma za kibenki kwa benki hizo kungeweza kuhatarisha usalama wa amana za wateja wake. Benki Kuu pia ilitoa utaratibu kwa mabenki wa namna ya kutekeleza Kanuni za Kimataifa za Utoaji Taarifa za Fedha, 9 (*International Financial Reporting Standard 9)* kuanzia mwezi Januari 2018.

Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017/18, mifumo ya malipo iliendelea kufanya kazi kwa ufanisi. Matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa kuhamisha fedha kutoka katika akaunti ya benki moja hadi nyingine (*Tanzania Automated Clearing House*) uliopo Benki Kuu uliendelea kutumiwa na Serikali katika kulipa mishahara na hivyo kuongeza ufanisi wa malipo. Aidha, mfumo wa malipo wa Benki Kuu ya Tanzania (Tanzania Interbank Settlement System – TISS) na ule wa Afrika ya Mashariki (*East Africa Payment System - EAPS*) iliendelea kufanya kazi kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa miamala ndani ya mifumo hiyo. Vilevile,

miamala inayotumia simu za mikononi baina ya mitandao ya simu katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017/18 ilikuwa milioni 44.8 ikiwa na thamani ya shilingi bilioni 1,905.2, ikiwa ni ongezeko la asilimia 92.7 ikilinganishwa na thamani iliyopatikana katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia. Hadi kufikia mwezi Desemba 2017, Watanzania wapatao milioni 19.3 walikuwa watumiaji hai wa miamala kwenye mfumo wa malipo kupitia simu za mikononi, ikilinganishwa na Watanzania milioni 17.02 waliokuwepo mwishoni mwa mwezi Desemba 2016.

***Zanzibar***

Katika kipindi cha robo tatu za mwanzo za mwaka 2017, pato la Taifa la Zanzibar lilikua kwa wastani wa asilimia 6.4 ikilinganishwa na asilimia 7.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa shughuli za utalii hususan malazi na huduma ya chakula; utawala; madini; na viwanda. Uchumi unatarajiwa kuendelea kuimarika katika kipindi cha pili cha mwaka 2017/18, ukichangiwa zaidi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kuongezeka kwa huduma za kitaalamu kwenye kilimo, kuimarika kwa kilimo cha maua na mboga pamoja na utalii. Mfumuko wa bei umeendelea kubakia ndani ya tarakimu moja na kufikia asilimia 5.9 mwezi Desemba 2017 kutoka asilimia 5.4 mwezi Juni 2017, ukichangiwa zaidi na kuongezeka kwa bei za chakula kama mchele, unga wa ngano na samaki.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2017/18, mapato ya ndani ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 320.5, sawa na asilimia 96.2 ya makadirio ya makusanyo kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2017/18. Mapato yatokanayo na kodi yalikuwa shilingi bilioni 289.9, wakati mapato

yasiyotokana na kodi yalikuwa shilingi bilioni 30.6. Jumla ya matumizi ilikuwa shilingi bilioni 378.2; kati ya hizo, matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 298.3 na matumizi ya maendeleo shilingi bilioni 79.9.

Urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 34.4 katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2017/18, ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 26.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2016/17. Hali hii ilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nchi za nje, ikiongozwa na karafuu na utalii; pamoja na kuongezeka kwa uhamisho mali wa kawaida (*current transfers*).

## Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2017/18

### *Malengo ya Sera ya Fedha*

Ili kufikia malengo ya Serikali ya kuimarisha uchumi, Benki Kuu imeendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuwepo kwa utulivu wa bei na riba katika masoko ya fedha kama matayarisho ya kutumia mfumo wa utekelezaji wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu (*central bank policy rate*) katika kutoa mwelekeo wa sera ya fedha ili uendane na malengo ya kudhibiti mfumuko wa bei na ukuaji halisi wa uchumi. Kwa kuzingatia maendeleo ya viashiria mbalimbali vya shughuli za uchumi katika siku za hivi karibuni, malengo ya sera ya fedha ya mwaka 2017/18 yaliyoainishwa kwenye kitabu cha Mwelekeo wa Sera ya Fedha kilichochapishwa mwezi Juni 2017, yamefanyiwa marekebisho na malengo ya sasa ni kama ifuatavyo:

i. ukuaji wa wastani wa fedha taslimu usiozidi asilimia 10.7;

ii. ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) usiozidi asilimia 12.0;

iii. ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi usiozidi asilimia 11.5; na

iv. akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

***Utekelezaji wa Sera ya Fedha kwa Kipindi cha Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2017/18***

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2017/18, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea na sera ya kuongeza ukwasi kwenye uchumi kwa kutumia nyenzo zake mbalimbali. Hatua hii ilikusudia kuongeza ukwasi katika mabenki ili kusaidia kuboresha utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi ili kuendeleza shughuli mbalimbali za uchumi. Benki Kuu iliongeza ukwasi kwenye uchumi kwa kununua fedha za kigeni kutoka katika soko la ndani, kubadilishana fedha za kigeni (*foreign exchange swaps*) na benki za biashara, na kutoa mikopo ya muda mfupi kwa benki za biashara. Aidha, Benki Kuu ilishusha riba yake (*discount rate*) zaidi na kufikia asilimia 9.0 mwezi Agosti kutoka asilimia 12.0. Hatua hizi pamoja na hatua zilizochukuliwa katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2016/17 zilisaidia kuongeza ukwasi kwenye benki za biashara na kushusha riba katika masoko ya fedha. Riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya mabenki (*overnight interbank cash market rate*) ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 2.95 mwezi Desemba 2017 kutoka asilimia 4.08 mwezi Juni 2017 na asilimia 13.69 mwezi Desemba 2016. Vilevile,

riba za dhamana za Serikali zilipungua hadi kufikia wastani wa asilimia 8.19 mwezi Desemba 2017 kutoka asilimia 15.12 mwezi Desemba 2016. Aidha, riba za mikopo inayotolewa na benki za biashara imebakia kuwa juu kutokana na benki hizo kuweka tahadhari kubwa kwa wateja wanaoshindwa kurejesha mikopo yao kwa wakati (risk premium), hali iliyochangiwa zaidi na kuongezeka kwa mikopo chechefu.

Ukuaji wa mwaka wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (*extended broad money supply, M3*), umeimarika na kufikia asilimia 8.0 mwezi Desemba 2017 kutoka asilimia 1.7 mwezi Februari 2017 ambao ulikuwa ni ukuaji mdogo zaidi kuwahi kufikiwa. Aidha, ukuaji huu wa fedha bado uko chini ya lengo la asilimia 12, unaotokana na lengo la ukuaji wa Pato la Taifa la asilimia 7.0 na mfumuko wa bei wa asilimia 5.0. Pia, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi umeanza kukua na kufikia asilimia 1.7 mwezi Desemba 2017, ikilinganishwa na kupungua kwa wastani wa asilimia 1.5 katika miezi miwili ya Septemba na Oktoba 2017. Hata hivyo ukuaji huu bado ni mdogo ukilinganishwa na ukuaji uliowahi kufikiwa katika kipindi cha nyuma; sababu kubwa ikiwa ni tahadhari iliyochukuliwa na mabenki katika kutoa mikopo kufuatia ongezeko la mikopo chechefu; na mabenki kupendelea zaidi kuwekeza kwenye dhamana za Serikali.

Thamani ya shilingi ya Tanzania imeendelea kuwa tulivu kwa kipindi chote cha nusu ya kwanza ya mwaka 2017/18, kutokana na kuimarika kwa urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje. Katika kipindi hicho, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,241 hadi 2,250, ikilinganishwa na shilingi 2,180 hadi 2,194 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2016/17.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2017/18, malengo ya sera ya fedha ya ongezeko la fedha taslimu na akiba halisi ya fedha za kigeni chini ya mpango maalum kati ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Serikali kuhusu makubaliano ya utekelezaji wa Programu ya Ushauri wa Kisera za Uchumi (*Policy Support Instrument (PSI)*) yalifikiwa.

***Matarajio ya Uchumi***

Kufuatia mwenendo wa viashiria vya ukuaji wa shughuli za uchumi katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017/18, Pato la Taifa linatarajiwa kukua kwa asilimia 7.0 badala ya matarajio ya awali ya asilimia 7.1. Katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2017/18 na katika kipindi cha kati, ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuendelea kuimarika kuendana na matarajio ya hali nzuri ya hewa itakayoongeza uzalishaji wa chakula; kuboreshwa kwa uzalishaji wa umeme na huduma za usafirishaji; matarajio ya kuimarika kwa uchumi wa dunia; na kuendelea kutekelezwa kwa miradi iliyopo kwenye awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (*Second Five Year Development Plan, FYDP II*).

Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubakia ndani ya lengo la asilimia 5 katika nusu ya pili ya mwaka wa fedha 2017/18. Hali hii itachangiwa zaidi na kuimarika kwa uzalishaji wa chakula, uzalishaji wa umeme na muendelezo wa sera thabiti ya fedha na kibajeti, pamoja na kuendelea kuwepo kwa utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani na sarafu nyingine duniani.

Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje inatarajiwa kuongezeka na kufikia asilimia 4.2 ya pato la Taifa mwaka 2017/18, kutoka asilimia 2.8 ya mwaka 2016/17. Hali hii itatokana na matarajio ya kuongezeka zaidi kwa uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi ikilinganishwa na mauzo nje ya nchi, kufuatia utekelezaji wa miradi mikubwa ya Serikali. Aidha, nakisi hiyo ya urari inatarajiwa kuongezeka zaidi katika kipindi cha kati kutokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi iliyoainishwa chini ya awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II).

Katika nusu ya pili ya mwaka 2017/18, sekta ya kibenki inatarajiwa kuendelea kuwa imara, salama na yenye mitaji na ukwasi wa kutosha. Benki Kuu itaendelea kufuatilia benki za biashara zenye kiwango kikubwa cha mikopo chechefu na kuhakikisha benki zote zinatumia mfumo wa kuhifadhi taarifa za wakopaji wakati wa kutoa mikopo mipya ili kupunguza vihatarishi. Benki Kuu pia itafanya uchambuzi wa kina kuhusu matokeo ya utekelezaji wa maamuzi ya kuongeza mitaji kwa ajili ya kujikinga na vihatarishi vya kiutendaji, pamoja na nyongeza ya asilimia 2.5 ya uwiano wa mitaji ya mabenki na kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha.

Kuhusu mifumo ya malipo, Benki Kuu itaendelea na zoezi la kuunganisha taasisi za Serikali kwenye mfumo wa malipo wa Benki Kuu ya Tanzania (*Tanzania Interbank Settlement System*) ili kuongeza ufanisi katika malipo yanayofanywa na taasisi za Serikali. Vilevile, Benki Kuu itaendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Malipo (*National Payment Systems Strategic Framework - 2018 – 2028*) na kuifanya mifumo ya malipo nchini kuwa ya kisasa zaidi.

***Mwenendo wa Sera ya Fedha Katika Nusu ya Pili ya Mwaka 2017/18***

Katika nusu ya pili ya mwaka 2017/18, Benki Kuu itaendelea kutekeleza sera ya fedha yenye kuongeza ukwasi katika uchumi ili kuendeleza ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na shughuli mbalimbali za uchumi. Kwa kutumia nyenzo zake, Benki Kuu itaendelea kuangalia kwa ukaribu kiasi cha ukwasi kwenye mabenki (clearing balances) ili kuleta utulivu wa riba katika soko la fedha baina ya mabenki. Utulivu wa riba katika soko la fedha baina ya mabenki ni msingi katika kutekeleza mfumo mpya wa utekelezaji wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu (*central bank policy rate*) katika kutoa mwelekeo wa sera ya fedha badala ya kutumia fedha taslimu. Mfumo huu mpya wa sera ya fedha unalenga kuifanya riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya mabenki (*overnight interbank cash market rate*) kuwa karibu na riba ya Benki Kuu.

Katika kuhakikisha mfumo huu unafanya kazi kwa ufanisi, Benki Kuu imefanya maboresho ya uendeshaji wa soko la fedha baina ya mabenki na kufanya soko hilo kuwa la kisasa zaidi linalotumia mfumo wa kielektroniki ili kuongeza ufanisi na uwazi baina ya mabenki (*electronic platform for interbank cash market operations*). Benki Kuu pia imeandaa makubaliano ya uendeshaji ya soko la mikopo ya muda mfupi baina ya mabenki (*General Master Repurchase Agreement – GMRA*). Aidha, Benki Kuu imerekebisha na kuboresha mfumo wa dhamana kwa kuongeza wigo wa dhamana za Serikali zinazokubalika kisheria kutumika kama dhamana kwenye masoko ya fedha, tofauti na mpango wa awali wa kukubali dhamana zinazoiva chini ya siku 180, na kuanzisha mpango mpya unaokubali dhamana zote za Serikali zinazoiva siku zaidi ya 180.

Utekelezaji wa sera ya fedha chini ya mfumo mpya, riba ya Benki Kuu (Central bank policy rate), itaamuliwa na Kamati ya Sera ya Fedha (*Monetary Policy Committee*) na itatangazwa hadharani kwa wadau wote. Benki Kuu itachukua hatua mbalimbali ili kufanya riba baina ya mabenki kubakia karibu na riba ya Benki Kuu na hivyo kusaidia upatikanaji wa ukwasi wa kutosha unaowiana na malengo ya mfumuko wa bei na shughuli mbalimbali za uchumi.

**Hitimisho**

Utekelezaji wa sera ya fedha ya kuongeza ukwasi katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2017/18, umesaidia kuongeza ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na ujazi wa fedha. Katika nusu ya pili ya mwaka 2017/18, Benki Kuu itaendelea na sera ya fedha ya kuongeza ukwasi katika uchumi, sambamba na kuhakikisha kwamba riba katika soko la fedha zinabakia tulivu, na ukuaji wa ujazi wa fedha unawiana na lengo la mfumuko wa bei wa asilimia 5.0, pamoja na matarajio ya ukuaji wa uchumi wa asilimia 7.0. Katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2017/18 na katika kipindi cha kati ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuendelea kuimarika kutokana na matarajio ya kukua kwa uchumi wa dunia, hali nzuri ya hewa itakayoongeza uzalishaji wa chakula, kuimarika kwa uzalishaji wa umeme na huduma za usafirishaji, na kuendelea kutekelezwa kwa miradi ya Serikali iliyopo kwenye awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (*Second Five Year Development Plan, FYDP II*).

Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubakia ndani ya lengo la asilimia 5 katika nusu ya pili ya mwaka 2017/18. Hali hii itachangiwa

zaidi na kuimarika kwa uzalishaji wa chakula nchini, uzalishaji wa umeme na muendelezo wa sera thabiti ya fedha na kibajeti, pamoja na kuendelea kuwepo kwa utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani na sarafu nyingine duniani. Aidha, makubaliano baina ya nchi wanachama wa OPEC kuweka mpango wa kupunguza uzalishaji wa mafuta kwenye soko la dunia kunaweza kuleta athari za kuongezeka kwa mfumuko wa bei kwani bei ya mafuta inaweza kupanda. Hata hivyo, Benki Kuu itaendelea kuchukua tahadhari pamoja na hatua za kisera ili kuendeleza utulivu wa uchumi.

Katika hatua ya kujiandaa kutumia mfumo wa utekelezaji wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu (*central bank policy rate*) katika kutoa mwongozo wa sera ya fedha, Benki Kuu itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuhakikisha mfumo huu unafanya kazi kwa ufanisi wa hali ya juu. Utekelezaji wa mfumo huu unategemea ufanisi wa masoko ya fedha pamoja na mawasiliano kwa wadau juu ya hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Benki Kuu ili kutekeleza sera ya fedha.

Kutokana na hatua madhubuti za utekelezaji wa sera ya fedha, pamoja na Serikali kuendelea kuboresha mfumo wa ukusanyaji kodi na usimamizi wa matumizi ya Serikali, ni matarajio ya Benki Kuu kuwa malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2017/18 yatafikiwa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, 11884 Dar es Salaam
Simu: +255 22 2233328, +255 22 2233350, Nukushi: +255 22 2234060
Tovuti: http://www.bot.go.tz

Kimepigwa Chapa na Identity Promotion Ltd